




MUHTASARI WA MODULI YA MFUMO SHIRIKISHI WA UHAKIKI (PGS)

Umeandaliwa kwa kuzingatia mwongozo wa mafunzo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) ulioandaliwa na TOAM kwa kushirikiana na wadau wa PGS Tanzania



MAANDALIZI YA MAARIFA HAYA

- Nakala hii ni tafsiri ya kiswahili ya mwongozo wa mafunzo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) uliotengenezwa awali kwa lugha ya Kiingereza kupitia ushirikiano wa shirika la kilimohai Tanzania (TOAM) na IFOAM – Organics International.
- Mwongozo huo ulishirikisha wadau wa PGS nchini Tanzania kuchangia ujuzi na maarifa ya namna mfumo huu unapaswa kutekelezwa.
- Kupitia mradi wa kitovu cha maarifa Afrika Mashariki (KHEA), TOAM iliweza kutafsiri mwongozo wa mafunzo haya kwa lugha ya Kiswahili ili kurahisisha matumizi yake kwa wadau mbali mbali wa mnyororo wa thamani. iliunga mkono tafsiri ya mwongozo huu kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili, kama sehemu ya kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa maarifa kuhusu PGS.

UTANGULIZI KUHUSU MAARIFA HAYA

- Mwongozo huu wa Mafunzo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) ni sehemu ya mfululizo wa nyenzo za mafunzo unaojumuisha moduli tano, zilizolenga kuwajengea washiriki uelewa na uwezo wa kutumia Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) katika Kilimohai.
- Nakala hii imejikita katika moduli 4 inayoangazia kwa ujumla namna kiwango cha bidhaa za kilimohai cha Afrika Mashariki (EAOPS) kinavyotumika katika PGS.
- Nakala nyingine za mafunzo kwa ajili ya moduli zinazofuata zinapatikana kama sehemu ya mfululizo huu, hivyo watumiaji wanashauriwa kuzitumia kwa pamoja ili kupata maudhui kamili ya mafunzo ya PGS.

MODULI YA NNE


Utangulizi wa Viwango vya Kilimohai katika
Utekelezaji wa PGS

Muhimu: Seti hii ya nakala za mafunzo kwa moduli ya 1-5 inapaswa kutumika kwa kufuata mwongozo wa Mtaala wa Mafunzo ya PGS kwa Wawezeshaji (ToT), 2025

Utangulizi wa Viwango vya Kilimohai katika Utekelezaji wa PGS

Yaliyomo

- Lengo la kujifunza
- Viwango ni nini?
- Kiwango cha Bidhaa za Kilimohai cha Afrika Mashariki (EAOPS)
- Madhumuni ya EAOPS
- Zoezi la kujifunza kuhusu EAOPS (Dakika 60)
- Matumizi ya EAOPS katika PGS





Lengo la kujifunza:

Kuwatambulisha washiriki kuhusu EAOPS ili waweze kuelewa mahitaji ya kiwango hicho na kuyatumia katika utekelezaji wa shughuli za PGS.

Kiwango ni Nini?

- Kiwango ni mwongozo unaoeleza jinsi bidhaa inavyopaswa kuzalishwa, kushughulikiwa au kuchakatwa.
- Kiwango cha Kilimohai kinaeleza mahitaji na taratibu zinazopaswa kufuatwa katika uzalishaji wa Kilimohai ili kuhakikisha uzalishaji unazingatia kanuni za Kilimohai.



Kiwango cha Bidhaa za Kilimohai cha Afri Mashariki (EAOPS)

- EAOPS ni kiwango cha Kilimohai kilichoandaliwa mahsusi kwa mazingira ya Afrika Mashariki.

Kiliandaliwa kwa ushirikiano wa wadau mbalimbali kupitia:

- Mashauriano ya kitaifa
- Majaribio ya matumizi ya shambani
- Ulinganisho na viwango vya Kilimohai vya kimataifa



Kiwango cha Bidhaa za Kilimohai cha Afrika Mashariki (EAOPS)..

Kiliandaliwa na Kikundi kazi cha Kikanda
cha Wataalamu wa Viwango (RSTWG) kwa
kutumia:

- Viwango vya Kilimohai vilivyokuwepo katika ukanda wa Afrika Mashariki.
- Viwango vya kilimohai vya kimataifa vya IFOAM.
- Mwongozo wa Codex Alimentarius kuhusu uzalishaji wa Kilimohai.



Kiwango cha Bidhaa za Kilimohai cha Afrika Mashariki (EAOPS)..

- EAOPS ni kiwango cha umma kinachosimamiwa na Mamlaka za Viwango za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Utekelezaji wa kiwango hiki unaratibiwa na

- Mashirika mwamvuli ya Kilimohai katika nchi za Afrika Mashariki.
- Kamati ya Pamoja ya Usimamizi katika ngazi ya kikanda (JMC)



Madhumuni ya EAOPS

- Kukuza uzalishaji na biashara ya bidhaa za Kilimohai katika nchi za Afrika Mashariki.
- Kutoa nembo ya pamoja ya kutambulisha bidhaa za Kilimohai na kujenga imani kwa walaji.

Kumbuka: EAOPS ilianzishwa sambamba na kuanzishwa kwa mfumo wa PGS katika Afrika Mashariki.

- Kutoa rejea katika kuandaa viwango, miongozo na kanuni nyingine za Kilimohai.
- Kurahisisha utambuzi na biashara ya bidhaa za Kilimohai katika masoko ya kikanda na kimataifa.

Matumizi ya EAOPS katika PGS:

Mambo Muhimu ya Kufahamu na Kufanya:

1. Orodhesha Shughuli Zako

- Mazao yote unayolima
- Mifugo yote unayofuga
- Bidhaa zote unazochakata
- Shughuli nyingine zinazohusiana na uzalishaji wako

2. Jifunze kuhusu viwango vya EAOPS

- Pata nakala ya EAOPS
- Soma mahitaji ya kiwango kwa kila shughuli unayofanya
- Tumia nyenzo za mafunzo zilizorahisishwa kuhusu uzalishaji wa mazao, mifugo na uchakataji wa bidhaa za Kilimohai.

Zoezi la 1: Chunguza na kujadili EAOPS ili kuona jinsi kanuni na taratibu za kikundi chenu zinavyoweza kuendana na mahitaji ya kiwango hicho.

Maswali ya Majadiliano

1. *Je, ni mahitaji gani ya EAOPS tayari yanatekelezwa katika kikundi chenu?*
2. *Je, ni maeneo gani yanahitaji kuboreshwa ili kuendana na EAOPS?*
3. *Je, ni hatua gani kikundi chenu kitachukua ili kuhakikisha kinazingatia EAOPS?*



Muda: Dakika 60

HITIMISHO

- Moduli hii imeangazia kwa ufupi namna kiwango cha bidhaa za kilimohai Afrika Mashariki kilivyoandaliwa na utekelezaji kupitia mfumo wa PGS.
- Kwa kutaka kuelewa Zaidi viwango hivi kwa kila wigo tembelea tovuti ya maarifa Afrika Mashariki na tafuta maarifa ya EAOPS.
- Katika Moduli ya 5 utajifunza zaidi kuhusu masoko ya kilimohai na namna ya kutambua fursa zilizopo na kuzitumia Pamoja na uendelevu wa PGS

*Imeandaliwa na Shirika Mwamvuli la Kilimohai Tanzania
(TOAM) kupitia mradi wa kitovu cha maarifa Afrika Mashariki
(Knowledge Hub for Organic Agriculture and Agroecology
Tanzania - KHEA)*

Kupata moduli nyingine tembelea jukwaa la kidijitali la maarifa ya
Kilimohai na kilimoikolojia katika tovuti: <https://khea-africa.org/>

Tunapatikana:

Mtaa wa Samora Avenue, Jengo la Kelvin House, gorofa ya Kwanza.
Kwa mawasiliano Zaidi tupigie kupitia +25574413499